# Mabadiliko ya Utabaka: Ulinganishi wa Riwaya za *Kuli* na *Pendo la Karaha*

*Virginia Wambui Mwathi, Vifu Makoti na John Mutua*
*Chuo Kikuu cha Machakos*

**Ikisiri**

**Utabaka hudhihirika katika jamii ya kibepari ambayo hugawanya watu kulingana na uwezo wao wa kumiliki na kudhibiti njia za uzalishaji mali. Marx anadai kuwa, historia ya jamii ndiyo historia ya mgogoro wa matabaka. Kutawaliwa kwa watu wa tabaka la chini na wale wa juu kunaeleza jumla ya muundo wa jamii. Jamii ina tabia ya kubadilika kadri ya mpito wa wakati. Kutokana na sifa hii, makala hii itachunguza mabadiliko ya utabaka katika jamii ya kibepari kwa kulinganisha matukio ya kitabaka katika riwaya za *Kuli* (Shafi, 1979) na *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014). Riwaya hizi zimeandikwa katika vipindi tofauti, *Kuli* imeandikwa katika karne ya 20 na *Pendo la Karaha* katika karne ya 21. Kwa hivyo, tunatarajia kuwa zitakidhi haja yetu ya kulinganisha ili kubaini ikiwa kuna mabadiliko yaliyokumba utabaka. Tunaamini kuwa utabaka ungalipo lakini kuna vipengele ndani yake vilivyobadilika kutokana na mpito wa wakati. Tutaongozwa na Nadharia ya Umarx iliyoasisiwa na Karl Marx na Friedrich Engels. Nadharia hii huonyesha migogoro ya kitabaka iliyopo katika jamii ambapo watu wa tabaka la chini hunyanyaswa na wale wa tabaka la juu. Tunatarajia kuwa utafiti huu utachangia katika fasihi ya Kiswahili na kuwa na umuhimu kwa wasomi katika viwango mbalimbali vya elimu na jamii kwa jumla.**

**Istilahi Muhimu**: *Utabaka, Tabaka, Ubepari, Nguvukazi*

## Utangulizi

Makala hii inachunguza mabadiliko yaliyokumba utabaka. Japo utabaka umekuwapo katika jamii kwa muda mrefu, kuna vipengele ndani yake vilivyobadilika. Tunanuiya kudhihirisha vipengele hivi kwa kulinganisha riwaya ya *Kuli* inayomulika kipindi cha ukoloni (karne ya ishirini) na riwaya ya *Pendo la Karaha (PLK)* inayomulika kipindi cha uhuru (karne ya ishirini na moja).

Mabadiliko ni hali inayokuwapo baada ya kutokea mageuzo fulani (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu,* 2004). Badiliko, ni jambo la kawaida katika maisha ya mwanadamu. Hutokea katika nyanja za uchumi, siasa na jamii. Vivyo hivyo, suala la utabaka katika jamii limekumbwa na mabadiliko.Tabaka hususan hubadilika kwa sababu za kiuchumi au mabadiliko ya utawala.

Utabaka katika jamii ya sasa, hauwezi kuzungumziwa bila kutaja utabaka mkongwe na wa sasa. Ule mkongwe, ulihusisha umwinyi na utumwa. Kwa sasa, utumwa haupo lakini umwinyi unadhihirika pale ambapo wasio na ardhi hutegemea wenye ardhi kwa kuuza nguvukazi zao kwao ama kukodisha ardhi zao ili kupata riziki (Odetola na Ademola, 1987). Kutokana na mabadiliko haya, imebainika kuwa, utabaka umekuwapo katika historia ya jamii.

Jamii tuliyomo kwa sasa, ni ya kibepari iliyoanza baada ya mapinduzi ya viwanda mwishoni mwa karne ya 18 na mwanzoni mwa karne ya 19 huko Ulaya. Jamii ya aina hii, ni ile inayowezesha watu wachache kumiliki rasilimali na njia kuu za uchumi wa nchi. Kutokana na sifa hii, ndipo utabaka unapodhihirika.

## Dhana ya Utabaka

Tabaka ni kundi la watu wenye hali moja linalotokana na jamii yenye mfumo wa kiuchumi ambao hugawanya watu kufuatana na uwezo wao wa kumiliki na kutawala njia za uzalishaji mali (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu,* 2004). *The Encyclopaedia Britannica, Vol. 10* inaeleza tabaka kama kundi la watu wenye hadhi sawa ya kiuchumi-jamii. *Kamusi Elezi ya Kiswahili* (2016) inaeleza tabaka kama kundi la watu wa jamii moja kimalengo au kiuwezo wa maisha. Katika makala hii, tunachukulia tabaka ni kundi la watu wenye sifa sawa za kiuchumi-jamii. Utabaka nao, ni ile hali ya kuwapo kwa matabaka

katika jamii. Ni mfumo wa ubaguzi ulio katika msingi wa kiuchumi-jamii. Mizizi ya utabaka ni ule ukosefu wa usawa katika ugavi wa mali na rasilimali unaosababisha jamii kugawanyika katika makundi tofauti na hivyo basi kukua kwa matabaka (Marger, 2017). Ukosefu wa usawa husababisha migawanyiko ya watu na migogoro (Wamitila, 2002).

**Mabadiliko ya Utabaka**

**Mabadiliko katika misingi ya rangi**

Utabaka katika misingi ya rangi ulidhihirika sana wakati wa ukoloni Barani Afrika. Wakoloni katika Afrika Mashariki walilazimisha itikadi za ukuu na utawala wa rangi yao kwa wenyeji wa eneo hili. Moja ya mifano mikuu ya utawala katika misingi ya rangi katika eneo la Afrika Mashariki ulikuwa ni tabia ya Waingereza ya kulazimisha Waafrika kufanya kazi hasa katika mashamba, migodi na viwandani. Mfumo huu wa nguvukazi ulithibitishwa katika misingi ya kuwa Waafrika walikuwa wanyonge na walifaa kupevushwa kwa kupewa kazi ngumu (Cooper, 2002).

Mfano mwingine katika eneo la Afrika Mashariki, ni kule kubaguliwa kwa Waafrika katika kupata huduma za kijamii. Sera ya utengaji huu ulikuwa katika misingi ya kuwa Waafrika walikuwa wanyonge na hawakufaa kuishi pamoja na Waingereza (Mamdani, 1996).

Hata katika elimu, Waafrika walifunzwa stadi za kimsingi tu kama kusoma, kuandika na ufundi huku Waingereza wakipata elimu pana (Mudimbe, 1988). Waafrika waliopata elimu pana walikuwa wachache sana kama vile wana wa machifu na viongozi wengine wa Kiafrika. Kipindi cha baada ya uhuru kimeshuhudia kupungua kwa utabaka katika misingi ya rangi. Kwa sasa, Mwafrika anamtawala na kudhulumu Mwafrika mwenzake. Wapo Waafrika wanaomiliki mali kwa wingi kama vile mashamba, magari, vipande vya ardhi, huku wengine hawamiliki chochote. Waafrika wengine wanaepuka mkono mrefu wa sheria kwa kufisidi wanasheria huku wengine wakinyimwa haki kutokana na unyonge wao. Katika mazingira ya kazi vilevile, wapo Waafrika ambao ni wasimamizi na mameneja na wanasimamia Waafrika wenzao.

Katika riwaya ya *Kuli (*Shafi, 1979), inayomulika kipindi cha ukoloni, tunapata tukio la George ambaye ni Mkuu wa kampuni ya Smith Mackenzie ambayo ni Kampuni ya mabepari inayomiliki gati ya Unguja. Yeye ni Mzungu. Ana asili ya Uingereza. Kazi yake ni kusimamia makuli wanapofanya kazi (kur. 60-61). Tabia yake ya unyanyasaji inatokea pale anapokosa kusikiza kilio cha wafanyakazi wake. Kilio hiki kinahusu nyongeza ya malipo, malipo kwa kufanya kazi saa za ziada na dhamana kwa kila mfanyakazi.Wanaposusia kazi, mwandishi anatueleza:

> ...George alivuta simu na kupiga ili kuita polisi. Haikuchukua muda mara kundi la polisi lilifika...
>
> (uk.163)

Tunamwona pia Kamishna ambaye ni Mzungu amewafungia makuli kadhaa waliokuwa wakigoma katika seli. Mmoja wao ni Rashidi. Kamishna anatishia kuwafunga Ubwa na Chum wanaokuja kutetea waliofungwa. Tunapata mfano ufuatao:

> "Ile wenzenu haitoki na kama ile watu mingine nafanya fujo na wao takwenda *jail* vilevile!"...*Listen you fools!* Wale wenzenu haiwezi kutoka mpaka kwa amri ya Bwana Resident...
>
> (uk. 92) Riwaya ya *Kuli*

Haya ni maneno ya Kamishna akiwaongelesha Chum na Ubwa. Kwa maoni yetu, huu ni ubaguzi katika misingi ya rangi kwa sababu, Kamishna angetatua ugomvi uliokuwapo kati ya makuli na wakuu wao kwa kusikiliza upande wa makuli na wakuu wao. Angepata George ana makosa pia kama mkuu na angechukua hatua yenye haki. Kwa hivyo, inabainika kwamba, dhuluma wanayopitia makuli ambao ni Waafrika chini ya Wazungu inadhihirisha kuwa katika jamii hii, rangi ya mtu inamweka katika tabaka maalum. Waafrika ambao ni wafanyakazi wanajipata katika tabaka la chini huku Wazungu ambao ni watawala na wakuu katika mazingira ya kazi, wakiwa katika tabaka la juu. Hii ni kusema kuwa, utabaka katika kipindi cha ukoloni, kinachomulikwa na riwaya ya *Kuli*, uko katika misingi ya rangi. Rangi ya mtu ni kiashiria cha tabaka lake.

Tofauti na haya, tunaona katika riwaya ya *Pendo la Karaha,* Saumu ambaye ni Mwafrika ni msimamizi katika *massage parlour* ya Fauziya. Tunaamini kuwa Saumu kama Mwafrika, atawapokea wafanyakazi wake wenye asili ya Kiafrika kama vile Kudra na Rose kwa moyo wa dhati na kuishi kwa pamoja kazini bila ugomvi. Badala yake, anachukua pasi zao na kuzificha na hata kukataa kuzirudisha wanapozihitaji. Hii ni njia ya kufanya waishi katika kazi ile kwa vile ni vigumu kuhama bila pasi. Tunaelezwa kuwa,

> "...pasi yako lazima uitoe," Saumu alisema... Kudra aliitoa pasi yake na akamkabidhi Saumu.
>
> (uk.165)

Zaidi ya hayo, anamlazimisha Kudra kufanya kazi asiyoipenda ya kukanda viungo. Saumu anampiga Kudra makofi na viboko anapokosa kula na na kukataa kazi. Amwambia Kudra,

> "Lazima utaifanya. Ikiwa hutaki kuifanya, nitakufanya uifanye!..."Ukichagua kazi ni shida yako. Mimi sitavumilia kiburi chako, unasikia?"
>
> (kur. 165-166) Riwaya ya *Pendo la Karaha*

Tabia ya Saumu inadhihirisha kuwa katika kipindi cha baada ya ukoloni, rangi ya mtu si kiashiria cha tabaka la mtu kama ilivyokuwa wakati wa ukoloni. Hii ni kwa sababu Saumu ni Mwafrika anayewanyanyasa Waafrika wenzake kutokana na uwezo alionao na hadhi yake ya kikazi bali si kutokana na rangi.

Katika umiliki wa mali, riwaya ya *Kuli* inatupa mfano wa Baniani anayemiliki duka la rehani. Yeye huwakopesha watu pesa wanapopeleka bidhaa zao na kuziweka rehani. Wanapolipa pesa, huzilipa kwa riba. Wateja wake wengi ni Waafrika kama vile Rashidi (kur. 53-55) ambaye yeye na mamake ni maskini na wanamtegemea Baniani katika hali ile ili kupata mahitaji yao ya kimsingi kutokana na mkopo atakaowapa. Kando na hayo, tunapata taswira ya nyumba ya kitajiri ya Morarji. Ina lango kubwa, ukumbi wake unang'ara kwa mataa ya umeme na ina jukwaa lililotandikwa kwa mito laini kabisa (uk. 50). Kwa upande mwingine, tunapata taswira ya nyumba ya Majaliwa ambayo si nyumba bali ni banda tu lililokandikwa dongo za kuezekwa makuti, halina dari na huvuja wakati wa masika (uk.16). Mifano hii inazidi kudhihirisha namna rangi ya mtu inavyomweka katika tabaka fulani. Katika kipindi cha ukoloni, Mwafrika ambaye ni mweusi anajipata katika tabaka la chini. Mwandishi amemhusisha na umaskini huku Baniani na Morjaji ambao ni wa rangi nyeupe wakiwa katika tabaka la juu na kuhusishwa na utajiri.

Tofauti na hayo, katika riwaya ya *Pendo la Karaha,* tunapata mhusika Rehema ambaye ni Mwafrika kutoka Mombasa nchini Kenya. Ana biashara ya kunadi wasichana kwenda ng'ambo. Biashara hii imemfanya tajiri. Nyumba yake ni ya kitajiri. Ina makochi spesheli, chetezo cha kufukiza ubani, friji mbili, chombo cha muziki na televisheni (uk. 82). Vilevile, ana mabasi (uk. 56). Rehema hajali kuwa wasichana anaonadi wanaenda kutesekea nga'mbo kwa kuchapwa, kunyimwa mishahara na kutusiwa. Kwa upande mwingine, tunapata taswira ya Kudra na mamake (Riziki) ambao pia ni Waafrika. Wao ni maskini. Riziki ana biashara ndogo ambayo haiwezi kukidhi mahitaji yao yote hasa karo ya Kudra (uk. 2). Hali hii inamlazimu Kudra kwenda kumwona Rehema ili amsaidie kupata ajira ng'ambo (uk. 64). Riziki ana wasiwasi na nyumba yake ambayo inavuja kuliko hapo awali. Hana uwezo wa kuhama kwa vile hawezi kumudu kodi za juu za mji wa Mombasa (uk. 101). Riwaya hii inadhihirisha kuwa katika kipindi cha uhuru, rangi ya mtu si kiashiria cha tabaka lake kama ilivyokuwa wakati wa ukoloni. Kwa sasa, yupo Mwafrika tajiri kama Rehema na yupo Mwafrika masikini kama Kudra na mamake. Aidha, yupo Mwafrika ambaye amechukua tabia za wakoloni kama vile ukatili. Mfano wake ni Rehema asiyejali maslahi ya Waafrika wenzake anaonadi. Kwa hivyo, uwezo wa mtu na umiliki wa mali unamweka mtu katika tabaka fulani tofauti bali si rangi yake kama inavyoonyeshwa katika riwaya ya *Kuli.*

Kutokana na haya, imebainika kuwa utabaka katika misingi ya rangi umebadilika na kuwa, kando na mtu wa rangi nyeupe kumnyanyasa Mwafrika, Mwafrika anamnyanyasa Mwafrika mwenzake kwa sasa.

**Mabadiliko ya Uhusiano wa Tabaka la Juu na la Chini**

Matabaka huhusiana kwa njia chanya na hasi. Katika dhana hii, tumepata mabadiliko katika mahusiano ya kitabaka kutoka utumwa wa kulazimishwa kwenda utumwa wa hiari. Matukio ya unyanyasaji yamekuwapo katika jamii. Mara kwa mara, watu hunyanyaswa bila hiari yao kwa mfano kupokonywa ardhi, kubakwa, kupigwa na kadhalika. Kwa upande mwingine, kuna visa vya watu kunyanyaswa kwa hiari yao kwa mfano kukubali kuajiriwa katika kampuni inayolipa mshahara mdogo sana usiolingana na kazi inayofanywa. 'Utumwa wa kulazimishwa' tumeuchukulia kwa maana ya namna ambavyo watu hunyanyaswa bila hiari yao na 'utumwa wa hiari' ukiwa na maana ya kukubali kufanyiwa matendo yaliyo kinyume cha haki ilimradi tu upate riziki.

Utumwa wa kulazimishwa unadhihirika kwa kiasi kikubwa tunapotazama kipindi cha ukoloni katika nchi za Afrika Mashariki. Tunasema ni wa kulazimishwa kwa vile wakoloni walienda nchi hizi na kuwanyanyasa wenyeji wa nchi hizi. Ukoloni ulianza mwishoni mwa karne ya kumi na tisa (19) hadi miaka ya sitini (60) ya karne ya ishirini (20). Mkoloni alimpokonya Mwafrika ardhi ambayo ni rasilimali yenye thamani na ya msingi zaidi iliyompa riziki na haiba, hivyo Mwafrika akakosa namna ya kuzalisha mali na kulazimika kuwa mtumwa nyumbani kwake kwa kumtumikia mkoloni Mzungu ili kupata riziki (Fanon, 1963). Huu ni mfano wa moja ya matendo ya unyanyasaji wa wakoloni. Mfano mwingine ni ule wa Waafrika kulazimishwa kufanya kazi katika mashamba ya wakoloni na tendo hili likaendelea hadi miaka ya sitini (1960) ambapo nchi hizi zilianza kupata uhuru (Mamdani, 1996). Nchini Kongo, wakoloni waliokuwa wenye asili ya Kibelgiji walinyonya madini ya nchi hii, kama vile dhahabu, kwa kuyasafirisha kwenda nchi yao (Hochschild, 1998). Kwa maoni yetu, yote hii ni mifano ya utumwa wa kulazimishwa. Hakuna apendaye kupokonywa mali yake na kulazimishwa kufanya kazi. Matendo ya Waafrika ya kupigania uhuru yanadhihirisha kupinga matendo ya kikatili ya hawa wakoloni.

Katika riwaya hizi, imebainika kuwa kuna mabadiliko ya utabaka kutoka utumwa wa kulazimishwa kwenda utumwa wa hiari kwa mujibu wa riwaya teule. Riwaya ya *Kuli* inadhihirisha utumwa wa kulazimishwa kutokana na uongozi na utawala wa Kiingereza katika jamii hii ya Zanzibar. Kuwapo kwa kampuni ya Smith Mackenzie inayomilikiwa na mabepari Waingereza katika ardhi ya Mwafrika, mkuu wake akiwa ni George ambaye ni Mwingereza, ni mfano wa utumwa wa kulazimishwa (kur. 60-61). Tendo la wafanyakazi hawa ambao ni Waafrika kutetea nguo za kazi, nyongeza ya mishahara, kulipwa kwa saa za ziada na dhamana kamili ya maisha kwa kila mfanyakazi linadhihirisha kuwa, wanapinga kunyanyaswa kazini (kur. 64-65). Dondoo lifuatalo linaonyesha madai yao:

> "...tunadai tupatiwe nguo za kazi, vilevile tunadai kila mfanyakazi awe na dhamana kamili ya maisha yake, kwani mara nyingi hapa bandarini wafanyakazi wanafikiwa na ajali na kampuni haichukui hatua yoyote..."
>
> (uk. 65)
>
> Wafanyakazi hawa wanafurushwa na askari, wengine wao wakikamatwa wakiwa mkutanoni unaohusu kutetea maslahi yao (kur. 85-86 na kur.183-184). Vilevile, wanapigwa na askari wanaposusia kufanya kazi kutokana na kilio chao kutosikizwa (kur.164-165). Haya, yanadhihirisha kuwa serikali ya kikoloni inawalazimisha wafanyakazi Waafrika kufanya kazi katika hali zinazowadhulumu na ambazo hawazitaki. Tunaelezwa kuwa, ... Kulikuwa hakuna ruhusa ya kusoma gazeti lolote lile isipokuwa yale yenye kutetea mawazo ya kikoloni tu na watu walikuwa hawana ruhusa ya kuonekana nje baada ya saa mbili za usiku.
>
> (uk.167) Riwaya ya *Kuli*

Hii inaonyesha kuwa serikali hii inajaribu kila iwezalo kuhakikisha kuwa Waafrika hawana muda wa kuungana na kuwasiliana kuhusu matatizo yao chini ya uongozi huu. Hii inamaanisha kuwa, serikali inawalazimisha kuishi namna ipendavyo bali si wapendavyo wao. La kusikitisha ni kuwa, hali

ambayo serikali hii inataka wenyeji waishi ni ya dhuluma. Ni hali inayodhihirika katika mazingira ya wafanyakazi wa bandarini wanaponyimwa nguo za kazi na kulazimishwa kufanya kazi kwa saa za ziada bila malipo. Aidha, kulipwa mshahara mdogo usiolingana na kazi wanayoifanya na kutopewa dhamana kamili ya maisha kwa kila mfanyakazi (kur. 64-65).

Riwaya ya *Pendo la Karaha* inadhihirisha kuwapo kwa utumwa wa hiari. Mwandishi anatueleza kuwa, Kudra anakamia kwenda nchi za ng'ambo kutafuta ajira ili ajikomboe kutoka kwa umaskini. Mamake anamweleza kuwa,

> "Wapo wasichana wanaotaabika katika miji kama vile Jeddah, Dubai, *New York, Berlin* na Cairo." Hili halikumpigisha mshipa Kudra
>
> (kur. 19-20)

Rukia anapouawa na mwajiri wake kule Dubai, Kudra anashtuka lakini baadaye anasahau na kurejea katika harakati za kutafuta nafasi ya kwenda ng'ambo kufanya kazi (uk. 50). Hapa ni anaporudi kwa Rehema kutafuta msaada. Tunaelezwa kuwa,

> Kudra akapata kusahau kadhia ya Rukia ya Dubai hata akarudi kwa Rehema kwa msaada... hata Riziki aliyasahau. Mwanzo, ndiye aliyemzuia Kudra kwenda Ughaibuni kutafuta maisha. Leo, ndiye aliyemshinikiza!
>
> (uk. 64) Riwaya ya *Pendo la Karaha*

Kule Dubai, ingawa Kudra anapata pesa zinazoinua maisha yake na ya mama yake kama alivyotamani, anateseka kweli kweli. Chini ya waajiri wake wa kwanza ambao ni Aminii na Nayrat, ananyimwa mshahara wake, anachapwa, anatusiwa, analazwa stooni na hata kupewa chakula cha makombo. Mwajiri wake wa pili Salim, anamtumia kama chombo cha anasa bila Kudra kupinga kwa vile anataka kudumisha ajira yake. Anapotoka kwa Salim, anahiari kufanya kazi katika kituo cha wazee na hata ufuoni, kazi inayodhalilisha sana. Lengo lake ni kupata riziki. Ifahamike kuwa, yeye ndiye aliyejitakia kwenda ng'ambo hata baada ya kusikia mateso wanayopitia wasichana wengine katika nchi hizo. Kwa hivyo, kujitakia kwake kuteseka ilimradi apate riziki, na mamake kumshinikiza kwenda ng'ambo kutafuta ajira, licha ya kuwa na ufahamu wa mateso wanayopitia wasichana, ni mfano wa utumwa wa hiari.

Pamoja na hayo, tunaamini kuwa, serikali inachangia kwa hiari katika kujipata katika utumwa miongoni mwa wananchi wake kwa: Kufumbia matendo ya Rehema macho ya kunadi wasichana wanaoenda kuteseka katika nchi za ng'ambo. Pia, kutomchukulia hatua ya kisheria mwajiri wa Rukia anapomuua Rukia. Aidha, serikali za Kenya na Dubai hazijali maslahi ya wasichana wafanyao kazi Dubai.

Mifano tuliyodondoa kutoka kwa riwaya za *Kuli* na *Pendo la Karaha* imebainisha kuwa, katika mifumo yote ya utumwa, mfanyakazi huonekana kuwa mnyonge. Nguvukazi yake haithaminiwi na mara kwa mara hupata malipo duni. Utumwa wa kulazimishwa umedhihirika sana katika kipindi cha ukoloni, na kwa kiwango kikubwa, uko katika misingi ya rangi. Mwafrika anateswa akiwa nyumbani kwake na anayemtesa ni mgeni kutoka bara lingine.

Utumwa wa hiari unatokana na haja ya kutoroka umasikini katika bara la Afrika na ukosefu wa ajira. Utafiti huu umebaini kuwa utabaka ungalipo. Tofauti iliyopo ni kuwa, kuna badiliko la kutoka kwa watu kunyanyaswa bila hiari hadi kunyanyaswa kwa hiari yao, ili kupata riziki. Watu hawajali yanayowatendekea katika mchakato wa kupata riziki, la muhimu ni wao kupata wanalolitafuta. Ndipo Waingereza wanaposema, *"The end justifies the means."*

**Mabadiliko katika Idadi ya Matabaka**

Tunapolinganisha kipindi cha ukoloni na baada ya ukoloni, kumekuwapo na mabadiliko muhimu sana katika idadi ya matabaka. Katika kipindi cha ukoloni, matabaka yaliamuliwa na rangi ya mtu na kabila lake huku katika kipindi cha uhuru, kumejitokeza matabaka mapya katika misingi ya elimu, kazi, mapato na hata uwezo wa kisiasa (Dirks, 2001). Kwa mfano, kuzuka kwa tabaka la kati nchini Nigeria, kumehusishwa na kukua kwa kiwanda cha mafuta na kukua kwa taaluma mpya na tabaka jipya la umeneja (Osaghae na Suberu, 2005).

Katika utafiti huu, tumegundua kuwa kuna kuongezeka kwa idadi ya matabaka katika kipindi cha uhuru ikilinganishwa na kile cha ukoloni. Mwandishi wa riwaya ya *Kuli* amedhihirisha matabaka mawili tu katika kipindi cha ukoloni. Msingi wa matabaka haya ni rangi ambapo Waafrika wanajipata katika tabaka la chini huku Waingereza na Mabaniani wakiwa katika tabaka la juu. Aliye katika tabaka la juu anakuwa na uwezo mkubwa wa kudhibiti Waafrika ambao ni wafanyakazi. Uwezo huu unakuwa pia kiashiria cha utabaka. Mfano ni George ambaye ni Mzungu na ni mkuu wa kampuni ya Smith Mackenzie. Wadogo wake ni Waafrika ambao ni makuli katika kampuni hii. Kamishna vilevile ni Mzungu ambaye ni mtawala na hivyo basi yu katika tabaka la juu. Ukamishna unampa uwezo wa kukamata na kuwafungia korokoroni Waafrika (tabaka la chini) wanaogoma na yeye tena ndiye mwenye uwezo wa kuwafungulia. Kwa jumla, serikali ya jamii ya *Kuli* ambayo ni ya kikoloni iko katika tabaka la juu. Kwa hivyo, matabaka mawili yanadhihirika katika jamii hii: tabaka la chini linalohusisha Waafrika ambao ni wafanyakazi na tabaka la juu linalohusisha watawala na waajiri wakoloni.

Riwaya ya *Pendo la Karaha,* inadhihirisha ongezeko la idadi ya matabaka. Tukiongozwa na uchanganuzi wa Tyson (2006) wa matabaka, tunapata jumla ya matabaka manne ijapokuwa uchanganuzi wake unadhihirisha matano.

Tabaka la kwanza ni la chini kabisa ambalo linahusisha watu wasio na makaazi, hawana mali wanayomiliki na hawana imani ya maisha yao kuimarika. Mfano ni Riziki ambaye anaishi katika nyumba mbovu ya kukodisha inayovuja. Hana uwezo wa kuhama kwa vile nyumba za mjini Mombasa zinagharimu kodi ya juu sana. Kando na hayo, mwandishi anatueleza kuwa anamlea Kudra kwa ugumu sana kwa vile karo ya shule, vitabu na sare za shule ni kero kwake (uk. 2).

Tabaka la pili linalodhihirika ni la chini kadri. Hili ni la watu wa elimu ya chini sana na nafasi za chini za ajira. Watu wa tabaka hili hung'ang'ana kusaidia familia zao na huishi kwa hofu ya kutofaulu maishani. Mfano wake ni Kudra ambaye baada ya kidato cha nne, anatafuta vibarua jijini Mombasa bila kufanikiwa na mwishowe anapata nafasi ya kwenda Dubai anakofanya kazi za kudunisha chini ya waajiri tofauti. Licha ya changamoto nyingi, anafanikiwa kumtumia mamake (Riziki) pesa za kuimarisha maisha yake na yeye mwenyewe pia. Tunaelezwa kuwa:

> Riziki kwa upande wake, Mungu aliendelea kumuinua. Aliendelea kuogelea katika ulimwengu mpya hapo *New Horizons*... Alimwajiri msichana wa kumsaidia kazi...Riziki aliingia katika vyama na kufungua akaunti za benki. Lengo la kufungua akaunti hizi lilikuwa kumwezesha mwanawe kumtilia pesa hata kutoka Uarabuni.
>
> (uk.156)

Dondoo hili linadhihirisha namna Kudra alivyojikakamua kuimarisha maisha ya mama yake.

Tabaka la tatu ni la kati. Hili ni la watu walio imara kifedha, wana makaazi mazuri, magari na hata humudu kupeleka watoto wao shule bora. Mfano ni Rehema ambaye ni tajiri kutokana na biashara ya kunadi wasichana kwenda ng'ambo. Anamiliki mabasi, na vitu katika nyumba yake ni vya bei ghali. Pia, anamuokoa mwanawe kutoka kwa uraibu wa mihadarati kwa kumlipia pesa katika kituo cha urekebishaji wa tabia (uk. 102). Mfano mwingine ni Fauziya anayemiliki biashara ya ukandaji wa viungo. Katika biashara hii, ameajiri msimamizi na wasichana wengi kufanya kazi hii.

Kwa mujibu wa Tyson (2006) tabaka la kati hujihusisha na lile la juu na vilevile kuonekana kama la juu. Tofauti ni kuwa, tabaka la kati halihusishwi katika mchakato wa serikali wa kufanya uamuzi. Tabaka la kati huathirika kiuchumi kwa vile ni tabaka linalolipa ushuru uliofanyiwa uamuzi na lile la juu. Katika riwaya hii, Rehema na Fauziya wanategemea serikali inayotumia vyombo vya dola kuhalalisha matendo yao ya kikatili baada yao kutoa hongo. Kwa hivyo katika riwaya hii, tabaka la nne ambalo ni la juu baada ya lile la kati, ni serikali ambayo ni tabaka tawala, na kutokana na uwezo wake wa kisheria, matabaka yote yanaliheshimu kama tabaka tawala. Kutokana na uchanganuzi huu, tunashikilia kuwa utabaka ungalipo lakini kinachobainika ni kuwa, idadi ya matabaka imeongezeka katika kipindi cha baada ya ukoloni ikilinganishwa na kile cha ukoloni.

**Hitimisho**

Kuna mabadiliko ambayo yamekumba utabaka kwa kulinganisha kipindi cha karne ya ishirini (20) hasa cha ukoloni kinachomulikwa na riwaya ya *Kuli* na kipindi cha karne ya ishirini na moja (21) ambacho ni baada ya ukoloni kinachomulikwa na riwaya ya *PLK*. Rangi imejitokeza kama kiashiria cha utabaka na ingawa ni kiashiria kisicho na uzito mkubwa katika karne ya ishirini na moja (21) ikilinganishwa na ya ishirini (20). Hii ni kwa sababu, watu wa rangi sawa sasa wanadhulumiana, na wako katika matabaka tofauti ikilinganishwa na hapo awali. Mahusiano ya utabaka yamebadilika pia kutoka utumwa wa kulazimishwa kwenda utumwa wa hiari kutokana na matukio ya watu kukubali kutendewa mambo yaliyo kinyume cha haki za binadamu. Hii ni tofauti na hapo awali ambapo Waafrika walipinga ukoloni vikali na kutetea haki zao kama wafanyakazi. Mwisho, ni kuongezeka kwa idadi ya matabaka katika karne ya ishirini na moja (21). Hii ni kutokana na matabaka ya sasa kudhihirika kutokana na kiwango cha elimu ya mtu, utajiri na uwezo. Hii ni tofauti na karne ya ishirini (20) ambapo rangi ilifanya kuwe na matabaka mawili tu. Kwa sasa, matabaka yanayodhihirika ni kati ya manne na matano. Kutokana na mabadiliko haya, tunashikilia kuwa, utabaka ungalipo lakini ni vipengele kadhaa vilivyobadilika ndani yake.

**Marejeleo**


Adam, S. (1979). *Kuli.* Dar es Salaam: Longhorn Publishers

Chiduo, E. Et.al. (2016). *Kamusi Elezi ya Kiswahili*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Cooper, F. (2002). *Africa since 1940: The Past of the Present.* United Kingdom: Cambridge University Press

Dirks, N. B. (2001). *Castes of mind: Colonialism and the Making of Modern India.* Princeton: Princeton University Press

Fanon, F. (1963). *The Wretched of the Earth.* London: Penguin Books

Habwe, J. (2014). *Pendo la Karaha.* Nairobi: Moran Publishers

Hochschild, A. (1998). *King Leopold's ghost: A story of Greed, Terror, and Heroism in Colonial Africa*. Boston: Houghton Mifflin Harcourt

Mamdani, M. (1996). *Citizen and Subject: Contemporary Africa and the Legacy of Late Colonialism.* Princeton: Princeton University Press

Marger, M. (2017). *Race and Ethnic Relations: American and Global Perspectives*. Boston: Cengage Learning

Mudimbe, V. Y. (1988). *The Invention of Africa: Gnosis, Philosophy, and the Order of Knowledge*. United States of America: Indiana University Press

Odetola and Ademola (1987). *Sociology: An Introductory African Text.* Hong Kong: Macmillan Publishers

Osaghae, E. E., & Suberu, R. T. (2005). *A History of Identities, Violence and Stability in Nigeria* (Vol. 6). Oxford: Centre for Research on Inequality, Human Security and Ethnicity University of Oxford

*The Encyclopaedia Britannica* Volume 10

TUKI.( 2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Oxford University Press.

Tyson, L. (2006). *Critical Theory Today.* London: Routledge Publishers.

Wamitila, K. W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.